# Nakala ya Mbinu

## Kushirikisha Watu waliopitia ukatili wa Unyanyasaji wa Kijinsia, dhuluma na unyanyasaji wa kijinsia (SEAH)

Chapisho hili la rejeleo ni kumbukumbu ya haraka ya kuelewa mazoea mema wakati wa kuwashirikisha watu waliopitia ukatili aina ya SEAH katika utengenezaji wa sera. Inatoa orodha ya hoja muhimu na maswali ambayo mashirika yanapaswa kuuliza wakati wa kufanya kazi na watu waliopitia ukatili.

Watu waliopitia ukatili wanaweza kutoa michango muhimu katika utengenezaji wa sera juu ya unyonyaji wa kijinsia, ukatili na unyanyasaji wa kijinsia (SEAH). Walakini, ushiriki wa maana unahusisha watunga sera kutenda ipasavyo na kwa uwajibikaji ili kuhakikisha kuwa sauti na maoni ya watu waliopitia ukatili yanasikika bila kusababisha madhara zaidi.

### Kwa nini kushirikisha watu waliopititia ukatili?

- ✓ Mashirika yana jukumu la kimaadili ya kuchukua maoni na uzoefu wa watu waliopitia ukatili kwa umakini.
- ✓ Watu waliopitia ukatili ni wataalam kwa uzoefu na wanajua zaidi ya mtu yeyote kile kinachofanya kazi na kisichofanya kazi.
- ✓ Kuchangia sera na mabadiliko kunaweza kusaidia watu waliopitia ukatili kupona na kuwasaidia kujiona wanathaminiwa.
- ✓ Kushirikisha watu waliopitia ukatili kunaweza kuhakikisha kuwa kazi ni husika na yenye ufanisi.
- ✓ Wafanyakazi na mashirika yatakuwa bora katika majukumu yao wakati wataelewa SEAH kutoka kwa mtazamo wa watu waliopitia ukatili.

### Wakati gani wa kutoshirikisha watu waliopitia ukatili?

- ✗ Ikiwa watu waliopitia ukatili bado wako katika hali ya hatari kutoka kwa wahalifu.
- ✗ Ikiwa shirika lenu halina sera sahihi na taratibu za kukulinda na kuhakikisha usalama wa watu waliopitia ukatili pamoja na wapiga filimbi wakati wote wa ushiriki na baada ya kushirikishwa.
- ✗ Ikiwa kujishughulisha kutasababisha madhara au kuwaweka watu waliopitia ukatili katika hatari ya kuumizwa na wahalifu, jamii au serikali (Kwa mfano; Athari za kuongea kama kufungwa au kupoteza hadhi ya kisheria).
- ✗ Ikiwa ushiriki huo ni wa kunufaisha shirika na sio mtu aliye pitia ukatili.
- ✗ Ikiwa shirika lenu halina nia ya kujaribu kutekeleza mapendekezo kutoka kwa watu waliopitia ukatili.

Ufafanuzi muhimu:

Njia inayojikita kulenga mtu aliyepitia ukatili: Kuhakikisha kuwa juhudi za kuzuia ukatili na kutoa msaada hazina ubaguzi na zinaheshimu na kutanguliza haki, mahitaji na matakwa ya watu waliopitia ukatili; hasa vikundi ambavyo viko hatarini au vinaweza kulengwa haswa na SEAH.[1]

Njia inayoongozwa na watu waliopitia ukatili: Njia ambayo inawaandaa na kuwezesha watu waliopitia ukatili kuchukua jukumu la uongozi katika maisha yao wenyewe na katika harakati kubwa dhidi ya aina ya unyanyasaji au unyonyaji ambao wamevumilia na kushinda.[2]

Njia inayofahamishwa na kiwewe au hofu: Njia inayotambua athari zilizoenea za kiwewe na inaelewa njia zinazoweza kutatua. Hii ni pamoja na kutambua ishara na dalili za kiwewe; kuunganisha kikamilifu maarifa juu ya kiwewe katika sera, taratibu na mazoea na kulenga kikamilifu kuzuia hofu isirudi kutokea tena.[3]

Jedwali lifuataĺo lina maana au lengo la kuongoza mashirika kupanga namna ya kushirikisha waliopitia ukatili. Hii sio orodha pana lakini inakusudiwa kuwezesha kufikiria nini ushiriki wa waliopitia ukatili unahusu.

---

[1] Boezio, G., nd Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa la 2467 (2019) linaimarisha haki na uwajibikaji na linataka mtazamo wa unaozingatia watu waliopitia ukatili katika kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji unaohusiana na unyanyasaji wa kijinsia, 29 April 2019. Umoja wa Mataifa
https://slavefreetoday.org/journal_of_modern_slavery/v2i1a2_Rise_Unite_Support_Doing_No_Harm_in_the_AntiTrafficking_Movement_countryman_roswurm.pdf

[2] Countryman-Roswurm, K. (2015). Inuka, unganisha, msaada: Kufanya "hakuna madhara" katika harakati ya kupambana na biashara haramu. Jarida la Utumwa Leo: Jarida la Taaluma Kadha la Suluhisho la Usafirishaji haramu wa Binadamu, 2, 1. URL
https://slavefreetoday.org/journal_of_modern_slavery/v2i1a2_Rise_Unite_Support_Doing_No_Harm_in_the_AntiTrafficking_Movement_countryman_roswurm.pdf

[3] Mentalhealth.org (2015) Mtazamo unaozingatia Kiwewe na Hatua za Kukabili Kiwewe. Imapitiwa 04.08.20 URL
https://www.mentalhealth.org/get-help/trauma#:~:text=Recognizes%20the%20signs%20and%20symptoms,actively%20resist%20re%2Dtraumatization.%22

## Unda mazingira salama na yanayoweza kufikika



**Hakikisha hatua za ulinzi na usalama kwa watu waliopitia ukatili na wapiga filimbi.** Je, sera na taratibu zenu za ulinzi na usalama ni husika, za kisasa na zinafaa? Je, mnao utaratibu au mchakato wa kusaidia watu waliopitia ukatili ikiwa kuna taarifa zinatolewa wakati wa au baada ya ushiriki?

**Hakikisha mipango ya usalama inatekelezwa.** Je, umefanya tathmini kuhusu athari ya ushiriki? Je, umefanya kazi baina ya watu waliopitia ukatili na wafanyikazi au wawezeshaji kuhusu kuandaa mipango ya usalama  binafsi wakati na baada ya ushiriki?

**Hakikisha msaada unapatikana kwa watu waliopitia ukatili ikiwa wameathirika na chochote wakati wa mashauriano.** Ni huduma gani zinahitajika? Unahitaji kushihirikisha au kujumuisha nini? Je, umezingatia hatua maalum kwa watoto? Je, umefikiria jinsi huduma zitalipwa?

**Hakikisha unapata eneo lakufikika na mazingira ni rafiki na kuzingatia mahitaji ya wote.** Je unazingatia mahitaji ya watu waliopitia ukatili ambao wanatoka sehemu mbali mbali na wana aina ya mahitaji tofauti? Unawasaidiaje watu walipitia ukatili kuweza kusafiri ili kufika kwenye eneo la mkutano? Utasaidiaje wazazi wanaoutunza watoto, watu wenye ulemavu au vikundi vingine kuweza kushiriki?

**Hakikisha usiri na kutokujulikana.** Je, waathirika wako katika hatari ya kutambuliwa wakihudhuria na kushiriki? Je, kwenye kazi au taarifa ya kazi, unaficha utambulisho wowote na kuondoa vitu vyovyote vinavyotambua mshiriki kufuatana na uzoefu wake binafsi?

## Kushirikisha kwa usikivu, kujali, uelewa na kwa kutafakari.



**Michakato inapaswa kuongozwa na kubuniwa na watu waliopitia ukatili.** Je, umefikiria jinsi watu waliopitia ukatili wanaweza kuongoza na kuchukua majukumu katika kubuni ushiriki na sera na mipango kwa njia ambayo haileti madhara zaidi? Je, umewauliza watu waliopitia ukatili njia gani wanazopenda zitumike?


**Hakikisha washiriki wote wametoa idhini kuhusu ushiriki, na matumizi yoyote ya picha, nukuu au maandishi**. Je, umeelezea kile ushiriki unajumuisha na kuelezea maana ya kutoa idhini kwa njia ambayo waliopitia ukatili wanaelewa? Umeelezea kuwa mshiriki anaweza kuacha kujishughulisha wakati wowote? Umeelezea jinsi picha yoyote, nukuu au maandishi itatumika na ni nani atakayeziona? Je, kuna kazi yoyote itakuwa mtandaoni, au itachapishwa, au itawekwa wazi kwa watu wote?

**Eleza matarajio halisi kwa ukweli na njia iliyo wazi.** Je, unakuwa mkweli juu ya kile unaweza kufanikiwa na rasilimali na muda uliyonao? Je unakuwa wazi kuhusu kile kinachoweza  kutokea kwa kushiriki? Je, yule aliyepitia ukatili anaelewa jukumu lako na mapungufu yoyote yaliyopo? Je, umeagiza utapiga simu, utatuma ujumbe mfupi au utatuma habari? Ikiwa ndivyo, hakikisha unatimiza maagizo.

**Mawasiliano yanapaswa kuwa wazi na ya kirafiki kabla na baada ya mchakato**. Je, mawasiliano na waliopitia ukatili yanawafanya wajisike huru na wapate faraja? Umeelezea mchakato, nini kitatokea na ufuatiliaji wowote unahitajika? Je, sauti yako na lugha ya mwili yako ni rafiki? Je, umetafakari juu ya hisia zako binafsi za ubaguzi na upendeleo na jinsi gani inaweza kuathiri mawasiliano na watu binafsi?

**Weka njia nyingi tofauti kwa waliopitia ukatili kuchagua jinsi wanataka kushiriki.** Je, umezingatia njia tofauti za kuwashirikisha waliopitia ukatili (maandishi, sauti, sanaa n.k)? Je, aliyepitia ukatili anaelewa chaguzi tofauti ya majukumu mbali mbali au mchango ambao anaweza kuwa nao?

## Kuwa na nyenzo/rasilimali na uwezo wa kubadilisha mipango.



**Hakikisha una ukweli juu ya wafanyakazi na wahusika wanaohusika.** Je, unao wafanyikazi waliohitimu wa kutosha kusaidia ushiriki, haswa wakati wa kufanya kazi na watoto na watu wanaoishi na ulemavu? Je, umejumuisha kupata dharura kwa mabadiliko yasiyotarajiwa? Kama ikiwa aliyepitia ukatili atajiondoa dakika ya mwisho, lakini anataka kushiriki? Je, unaweza kupanga kipinidi kingine tena?

**Fikiria gharama ya ushiriki.** Je, unatoa chakula kwa washiriki? Je una gharama za ukumbi? Je unahitaji ukumbi wa vikao vidogo vidogo ? Je! Unahitaji watafsiri?

**Fidia za kifedha kwa manusura na wataalamu.** Je, Unawalipa waliopitia ukatili kwa wakati ?  Je, unalipia gharama zozote za usafiri na malazi (waliopitia ukatili wanaweza kuhitaji kuwahi mapema kufika mahali pa mkutano)? Je, unatoa gharama za utunzaji wa watoto au huduma ya watoto?